LAIKIPIA UNIVERSITY JOURNAL OF SOCIAL SCIENCES, EDUCATION AND HUMANITIES

# Udhalilishaji wa Asasi Kuu za Kijamii katika Muziki wa Kisasa

***Lucy Mugo***
Department of Literary and Communication Studies, Laikipia University, Kenya

**Abstract**
Pop music is one of the genres with the greatest appeal to the Kenyan youth, and it continues to impact them profoundly. Although this music is a form of entertainment for the youth, Contemporary Pop Music has been used as a platform for disseminating the youth's problems in society. From time immemorial, music has been used to highlight societal challenges. Therefore, this paper critically analysed how the youth has used Contemporary Pop Music to subvert entrenched customs, beliefs, and institutions in society. The study aligned itself with Jean-Francois Lyotard's idea of postmodernism which is rooted in the subversion of institutions and ideological forms of knowledge as instruments of oppression in the society since they have failed to capture the local realities. Using purposively selected 5 contemporary popular songs in Kenya, this article provides a textual analysis of how postmodernism styles used in the songs serve to subvert entrenched customs, beliefs, institutions, education, language, and religion as instruments of oppression. Challenging these established norms allowed the youth to express themselves freely through music. This study will help shed light on issues of concern to the youth and hopefully help policymakers by offering reference material for the formulation of policies and strategies that will address these issues. More specifically, the findings of this study will contribute to the field of discourse analysis in Kiswahili, literary linguistics, and Oral literature and will help linguistics and literature scholars as reference material in understanding contemporary pop music. Finally, this study will bring a new perspective to understanding contemporary pop music in our society.

**Keywords:** Contemporary pop music, established norms, postmodernism, subversion, youth

**Ikisiri**
Muziki wa Kisasa ni mojawapo wa muziki maarufu sana kwa vijana nchini Kenya. Licha ya kuwa kitumbuizo kwa vijana, muziki huu hutumika kama nyenzo ya kuwazindua vijana ambao wako kwenye shinikizo zito kutokana na matatizo yanayowakumba katika jamii. Tangu miaka na mikaka, binadamu amekuwa akitoa hisia zake: za uchungu, kero, mafadhaiko au furaha kupitia muziki ambao husawiri mazingira yake. Mintarafu ya hayo, makala haya yalichunguza jinsi muziki wa kisasa unatumika kudhalalisha asasi kuu za kijamii ambazo badala ya kutoa suluhisho la matatitzo chungu nzima yanayowakumba vijana, asasi hizi ndizo chanzo kuu cha matatatizo hayo. Mawazo ya Jean-Francois Lyotard katika nadharia ya usasaleo kuhusu udhalilishaji wa tamaduni na asasi kuu zinazokandamiza maisha ya watu kwani haziakisi hali halisi ya maisha yalikuwa dira katika uchunguzi huu. Muundo wa utafiti huu ulikuwa wa kiuthamano na kimaelezo na ulifanyika maktabani. Data ya msingi katika utafiti huu ilikuwa nyimbo tano za Genge ambazo zilipakuliwa mtandaoni. Makala haya yanaonyesha kwamba Muziki wa Kisasa umewapa vijana jukwaa la kudhalilisha asasi kuu kama vile dini, lugha na vyombo vya dola kwani vinawasababishia vijana mahangaiko mengi. Udhalilishaji wa asasi kuu katika tungo zao umewapa vijana njia salama ya kujikomboa kutokana na mifumo ya awali ambayo haikuwapa nafasi ya kujieleza wala kuruhusu mabadiliko. Matokeo ya utafiti huu

Volume 1, Number 1, 2024 ISSN N0 2791-190Xv

yatakuwa malighafi katika taaluma za isimu na fasihi pamoja na uchanganuzi diskosi matini Aidha matokeo ya utafiti huu yatotoa mwanga kuhusu maswala yanayowakumba vijana hivyo basi ni marejeleo muhimu kwa washika dau wote wanaobuni sera na mikakati kabambe ya kuwainua vijana ambao ni nguzo muhimu katika jamii.

**Istilahi kuu**: Asasi kuu, muziki wa kisasa, udhalilishaji, usasaleo, vijana

## Utangulizi

Vijana ni nguzo muhimu katika jamii na taifa kwa jumla tena wana nafasi kubwa ya kujenga jamii yao kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, jamii imeundwa kwa namna kwamba asasi kuu zinawakandamiza vijana huku watu walio na uwezo wakiendelea kuwadhulumu na kuwanyima haki. Ogutu (2021) anaelezea kuwa vijana wapo kwenye shinikizo zito linalowazuia kuafikia malengo na matamanio yao katika maisha. Hali hii imewalazimu vijana kutumia muziki wao kama jukwaa la kudhalilisha asasi kuu zinazowasababishia matatizo chungu nzima. Binadamu amekuwa akitoa hisia zake za uchungu, kero, mafadhaiko au furaha kupitia muziki. Kazi ya msanii ni kusawiri masuala yaliyomo kwenye jamii kama vile ukosefu wa kazi, unyonyaji, ukoloni mamboleo, uzalendo, usaliti, matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa mambo mengine yanayoikumba jamii (Wanjala 2016). Kutokana na hayo, muziki wa kisasa basi ni zaidi ya sauti tu ambazo huimbwa na kuchezwa. Muziki huu ni sauti na satua ya vijana katika kuelezea yanayowakumba katika jamii.

Licha ya kuwa watafiti wengi wamekuwa wakijikita katika mitindo na maudhui ya sanaa ya jadi, baadhi ya tafiti zinazohusu aina ya muziki huu (Kipsang, 2016; Koech, 2021; Kasyoka, 2022) zimejikita katika uhakiki wa masuala nyeti kama vile ngono pamoja na matumizi ya dawa za kulevya yanayodhihirika katika muziki huu. Kwa upande mwingine, udhihirikaji wa masuala hayo nyeti ni ishara ya upingaji na udhalilishaji wa tamaduni ambazo zimetawala mfumo wa maisha ya watu kwa muda mrefu (Mukasa, 2022). Ni dhahiri kuwa swala la udhalilishaji wa asasi kuu za kijamii katika Muziki wa kisasa limetiwa kapuni ilhali ni wazi kuwa muziki huu ni nyenzo maarufu ya kudhalilisha hali na asasi kuu katika jamii zinazowasababishia vijana masaibu mengi.

Dhana hii ya udhalilishaji wa asasi kuu ilifafanuliwa na Mfaransa Francois Lyotard (1979). Lyotard alipinga matumizi ya asasi kuu zilizokuwa zinakandamiza maisha ya binadamu. Hii ni kwa sababu asasi kuu hazina uhusiano wowote na hali halisi ya maisha. Kwa hivyo, Lyotard alipendekeza matumizi ya asasi ndogo ndogo zinazosimulia na kuakisi hali halisi ya maisha. Aidha, Lyotard anaelezea kuwa maendeleo ya viwanda yalibadilisha kwa kiwango kikubwa ufahamu wa jamii. Ufahamu huu umewapa wasanii kibali cha kuwasilisha hisia zao na za wanajamii wengine kuhusu hali zinazowakumba kwa kutumia nyenzo zinazokiuka kanuni zilizozoeleka za jadi na kuienzi mitindo ya kisasaleo.

Carter (2006) anahoji kuwa jaribio la kuelezea ukuaji wa jamii na tamaduni zake kwa kutumia asasi kuu na nadharia hazifai na hazikubaliki tena. Swala hili linaungwa mkono na Barry (2002) anayependekeza kuwa watu watumie urazini na umantiki ili kuleta suluhisho kwa matatizo ya kijamii. Kwa hivyo, ni wazi kuwa jamii haitegemei tena asasi kuu kuipa mwelekeo wa maisha. Walmsley (2006) anaonyesha kuwa udhalilishaji wa asasi hizi hulenga maana ya uasi dhidi ya kaida zilizopo au zilizokuwepo na kusababisha asasi hizi kufifia zenyewe. Hivyo basi, Muziki wa Kisasa umetungwa na kuimbwa kwa lengo la kudhalilisha asasi hizi. Aidha, Kipkemoi (2018) anafafanua kuwa nyimbo ni matini ambayo inaweza kuchanganuliwa jinsi zilivyo matini nyingine. Isitoshe kupitia kwa nyimbo, vijana wana nafasi kubwa ya kudhalilisha na kuhujumu mifumo na asasi zinazowasababishia matatizo mengi katika jamii.

Zaidi ya hayo, Wamitila (2006) anaelezea kuwa kutokana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kisayansi, kiteknolojia na kisanaa, sifa za nyimbo zilibadilika hasa baada ya karne ya ishirini na moja. Nyimbo hizi zilihusishwa na udhalilishaji wa simulizi kuu. Huelezea au kuzitambulisha sifa mpya za dhamira, tanzu, dhana na mitindo ya kifasihi inayohusishwa

Volume 1, Number 1, 2024 ISSN N0 2791-190Xv

na miongo ya kwanza ya karne ya ishirini. Mintaarafu ya hayo, nyimbo husika zilichunguzwa kutoka juu, chini, kulia na kushoto ili kubainisha asasi kuu ambazo zimedhalilishwa kwani zimehangaisha maisha ya vijana.

## Mapitio Ya Maandishi

Vijana wanaweza kutumika katika jamii ili kuleta mageuzi. Kiongera (2010) katika tasnifu yake alishughulikia mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya. Alionyesha kuwa vijana wanatambua maovu ya viongozi wa kisiasa ambayo yanawafanya wapitie maisha magumu. Alihitimisha kazi yake kwa kuonyesha jinsi vijana wamechangia katika kuleta ukombozi wa jamii. Utafiti wa Kiongera ni tunu kwa makala haya kwani ulisaidia kuonyesha vile vijana wana uwezo wa kutambua maovu ya viongozi na hivyo kutumika kuzindua vijana wengine ili waelewe hali halisi ya mambo katika jamii yao.

Utafiti wa Njoroge (2014) ulionyesha kwamba matatizo hasi yanayozikumba jamii za leo yamesababishwa na asasi kuu za kijamii. Aidha, mabadiliko hasi yanayoshuhudiwa katika nchi na jamii mbalimbali husababishwa na viongozi ingawa viongozi wanastahili kuwa mawakala wa mabadiliko chanya. Vilevile, lililodhihirika katika makala haya ni kwamba wanajamii kwa kutofurahia mabadiliko haya hasi, walijitetea kwa kuyakaidi hata ingawa wengi wao hawakufaulu. Ingawa utafiti wa Njoroge ulichanganua viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika riwaya, uliyafaa makala haya katika kuonyesha jinsi wasanii wa Muziki wa Kisasa wanavyopinga uongozi mbaya na kuwataka raia wajikakamue wabadilishe hali ilivyo.

Gromov (2022) anafafanua kuwa wasanii wa Muziki wa Kisasa wanapinga mifumo ya utawala ya nchi zinazoendelea ambayo wanaona haina neema yoyote kwa raia. Wasanii hawa huonyesha hasira zao kwa kile ambacho wao wanaona ni ujinga wa viongozi au serikali hizo kukubali kiholela masharti yanayowekwa na mataifa makubwa. Kwa mujibu wa wasanii hawa, kukubali kudanganyika kirahisi na mambo haya, kumesababisha kuporomoka vibaya sana kwa nchi zinazoendelea katika sekta zake zote. Hivyo basi kulingana na Gromov mataifa makubwa ni asasi kuu ambazo zinastahili kudhalilishwa ikiwa nchi zinazoendelea zitapata uhuru wa kijiamulia yanayozifaa. Aidha, anadhalilisha imani za usasa kuhusu maendeleo ya lazima katika hatua za maisha ya binadamu na yasiyojali athari zake kwa mazingira na kupendekeza maendeleo yanayozingatia uhifadhi wa mazingira. Mawazo haya yaliongoza makala haya.

Njeri (2018) anahoji kuwa vijana wana nafasi kubwa ya kupigania haki. Utafiti wake ulishughulikia mchango wa vijana katika kuleta ukombozi katika kazi za Leonard Sanja. Utafiti wake ulibaini kuwa vijana wanakumbwa na matatizo mengi yanayowalazimu kupigania haki zao. Utafiti huu ulikuwa hazina kwa makala haya katika kubainisha matatizo yanayowakumba vijana, jambo ambalo linawalazimu wanamuziki kutumia muziki wao kuwazindua vijana kuhusu hali hii.

Kipkemoi (2018) alichanganua jinsi simulizi za virusi vya ukimwi zinavyodhihirika katika nyimbo za jamii za Kenya kibaadausasa. Alihakiki jinsi miundo na taratibu za kijamii zilivyowezesha asasi kuwa na mamlaka na udhibiti kwa kuwatenga wanajamii wengine hasa wendawazimu, wagonjwa, wachochole, wahalifu na waliokiuka maadili. Isitoshe, alionyesha kuwa nyimbo katika muktadha wa baadausasa zina simulizi kuu na simulizi ndogo zinazolenga kujadili suala la VVU/UKIMWI. Aidha utafiti wake unadhalilisha nguvu za awali au zilizokuwa zinatawala kama zile za kisayansi na wanajamii kuhusu VVU/UKIMWI na waathiriwa na kuonyesha kuwa nyimbo zinaweza kuwa njia mbadala inayoweza kutumiwa kukabiliana na janga la UKIMWI. Kwa kuwa mbinu za kisayansi hazijafaulu kabisa katika vita dhidi ya VVU/UKIMWI, kuna haja ya kutumia mbinu anuwai zikiwemo za kitamaduni kama vile nyimbo pamoja na mbinu za kisayansi. Mawazo haya yake ya kupendekeza simulizi ndogo ndogo kama nyimbo yamekuwa dira katika makala haya.

Utafiti wa Njogu na Chimera (1999) ulionyesha namna wanariwaya kama S.A Mohamed, M.S Mohamed, S.A Shafi na George Orwell walivyomulika matatizo mbalimbali yaliyokumba


Received: 21-07-2024 Accepted: 20-10-2024 Published: 27-12-2024

Volume 1, Number 1, 2024 ISSN N0 2791-190Xv

jamii kwa kudhalilisha asasi kuu za kijamii. Katika utafiti wao, walionyesha jinsi matatizo hayo yangesuluhishwa kwa kutumia mapinduzi. Japo watafiti hawa walijikita katika riwaya, utafiti wao ulikuwa dira katika kuonyesha jinsi wasanii wametumia Muziki wa Kisasa kuwazindua vijana kuhusu matatizo yanayowakumba na kuonyesha jinsi matatizo haya yangesuluhishwa. Hivyo basi, utafiti wao ulipatia makala haya mwelekeo wa kutathmini udhalilishaji wa asasi kuu za kijamii katika Muziki wa Kisasa.

**Msingi wa Nadharia**

Udhalilishaji wa asasi kuu umechanganuliwa kwa kuzingatia nadharia ya Usasaleo. Dhana ya usasaleo hutumiwa kueleza uasi dhidi ya kanuni hususan zilizojikita katika kipindi cha usasa. Kulingana na nadharia hii, jaribio la kuelezea ukuaji wa jamii na tamaduni zake kwa kutumia asasi kuu na nadharia hazifai na hazikubaliki tena. Hii ni kwa sababu asasi hizi kuu hazina uhusiano wowote na hali halisi. Mawazo ya Jean-Francois Lyotard (1979) katika nadharia hii kuhusu udhalilishaji wa tamaduni na asasi kuu zinazokandamiza maisha ya watu kwani haziakisi hali halisi ya maisha yalikuwa dira katika makala haya. Lyotard anahoji kuwa simulizi ndogo ndogo huhusu 'vijihadithi' vinavyosimulia na kuakisi hali halisi ya maisha ya wanajamii.

Fauka ya hayo, Lyotard anaeleza kuwa katika sayansi, mbinu hii ya kutumia simulizi ndogo ndogo ni nyenzo kuu katika kusuluhisha matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hii ni kwa sababu mbinu hii huwawezesha kutafuta kweli kinzani, udhaifu na yasiyojulikana ambayo huwezekana kupitia simulizi ndogo ndogo ambazo zinakumba sehemu ndogo kuliko simulizi kubwa ambazo zinakumba ulimwengu mzima. Aidha, Lyotard anaelezea kuwa maendeleo ya viwanda yalibadilisha kwa kiwango kikubwa ufahamu wa jamii. Ufahamu huu umewapa wasanii kibali cha kuwasilisha hisia zao na za wanajamii wengine kuhusu hali zinazowakumba kwa kutumia nyenzo zinazokiuka kanuni zilizozoeleka za jadi na kuienzi mitindo ya kisasaleo. Hivyo basi, nadharia hii ilikuwa nguzo katika makala haya katika kuonyesha jinsi asasi kuu zinavyodhalilishwa katika Muziki wa Kisasa.

**Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Data ya msingi ya utafiti huu ni matini za nyimbo teule za Muziki wa Genge. Data yenyewe ilipakuliwa kutoka mtandaoni. Khakasa (2016) anahoji kuwa mtandao una rasilimali nyingi na hutoa fursa kubwa kwa watumiaji wake. Kila kitu kinaweza kupatikana kwenye wavuti ya ulimwengu. Mtafiti alitumia sampuli kusudio kuteua nyimbo tano za Genge ambazo ni: *Kuna Siku Youth Wataungana* ulioimbwa na Wakadinali, *Kwenda* ulioimbwa na Khaligraph Jones, *Khalicartel* ulioimbwa na Khaligraph Jones, *Tujiangalie* ulioimbwa na Sauti Sol na *Wajinga Nyinyi* ulioimbwa na King Kaka. Uteuzi huu ulizingatia nyimbo ambazo zinadhihirisha udhalilishaji wa asasi kuu za kijamii.

Nyimbo zilizoteuliwa zilikodiwa na kupangwa mintarafu ya madhumuni ya makala haya. Nyimbo hizo zilipewa nambari G1-G5, herufi G ikirejelea aina ya muziki: Genge. G1, *Kuna Siku Youth Wataungana*, G2 *Kwenda*, G3 *Khalicartel3*, G4 *Tujiangalie* na G5 *Wajinga Nyinyi*. Vilevile nyimbo hizi zilipangwa katika beti na kila mstari katika beti hizo ulipewa nambari. Aidha, data ya matini za nyimbo zilizoteuliwa iliyoakisi madhumuni ya makala haya, na ambayo ilikuwa katika lugha ya Sheng, Kiingereza na lugha zingine za mama ilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Newmark (1991) wanaeleza kwamba katika kazi ya kutafsiri, maana asilia ya maneno kutoka lugha chanzi ndiyo huzingatiwa.

**Matokeo ya Utafiti**

Makala haya yamebaini kuwa Muziki wa Kisasa umedhalilisha asasi kuu za kijamii. Kulingana na Lyotard (1979), asasi kuu ambazo aghalabu zimeundwa ili kusuluhisha matatizo ya watu ndizo zinakandamiza maisha ya binadamu. Hii ni kwa sababu simulizi kuu hazina uhusiano


Received: 21-07-2024 Accepted: 20-10-2024 Published: 27-12-2024

wowote na hali halisi ya maisha. Kwa hivyo, Lyotard alipendekeza matumizi ya simulizi ndogo ndogo zinazosimulia na kuakisi hali halisi ya maisha. Kutokana na hayo, ni wazi kuwa jamii haitegemei tena asasi hizi kuu kuipa mwelekeo wa maisha kwa hivyo asasi hizi zitafifia zenyewe. Udhalilishaji wa asasi kuu zilizochunguzwa katika makala haya ni pamoja na vyombo vya dola, elimu, lugha na utamaduni na dini.

**Vyombo vya Dola**

Vyombo vya dola ni asasi za kijamii zinazokabidhiwa jukumu la utawala na uongozi wa jamii hiyo. Makala haya yameng'amua kwamba vyombo hivi vya dola vinadhalilishwa na wasanii. Hii ni kwa sababu ingawa vyombo hivi vilibuniwa kwa madhumuni ya kusuluhisha matatizo ya jamii, vyombo hivi vimesababishia watu mateso na mahangaiko mengi sana. Vyombo vya dola vinavyokandamiza maisha ya watu ni kama vile polisi, mahakama na bunge.

**(i) Polisi**

Kulingana na katiba ya Kenya (2010), jukumu la huduma ya polisi ni kutoa ulinzi wa maisha na mali ya raia, kudumisha amani ya umma na hali nzuri, na kuzuia, kuchunguza na kutatua uhalifu kwa kuwaleta wahalifu katika mfumo wa sheria. Hata hivyo, kwa mujibu wa matini zilizochanganuliwa, makala haya yamebaini kuwa badala ya polisi kulinda raia, wanawasababishia mateso na mahangaiko mengi ndiposa asasi hii inadhalilishwa na wasanii kama inavyodhihirika katika matini ifuatayo.

**Matini 1**

**G3 *Khalicartel 3* (Ubeti 7, 7-8)**

*7. Hii upande hatunanga kitu si huishi daily [kila siku] na imani*
*8. Lullaby huku mtaa yukuwa ni sauti ya risasi* [bembelezi ya mtaa wetu ni sauti ya risasi]

**G5 *Wajinga Nyinyi* Ubeti 7 (12-17)**

*12. Petroli imepanda so inamaanisha polisi wata operate kama customer care* [Petroli imepanda kwa hivyo polisi watakuwa waelekezi wateja]
*13. Busaa na chwara zinamaliza mayouth*
*14. Wachane na polisi wafanye raid tena* [Polisi wavamie tena]
*15. Ama ni vile OCS hajapewa yake na kila mwizi*
*16. Oh, i mean ya kila mwezi* [samahani, ninamaanisha ya kila mwezi]
*17. Na polisi wako in cahoots, hao ndio uSupply wagondi na guns za ku shoot* [polisi ndio huwapa wahalifu bunduki]

**Ubeti 5 (8-9)**

*8. Wakinisnipe tonight si mnajua ni kwa nini* [nikishikwa leo usiku si mnajua ni kwa nini]
*9. Nitakufia watu mi siogopi mimi*

Kinachobainika katika matini hii ni kwamba wasanii wanadhalilisha idara hii ya polisi kwa kuwa badala ya kuwalinda raia, wanawadhulumu. Idara hii inalinganishwa na sehemu ya kuwasaidia wateja katika shirika au kampuni ambapo huduma bora zafaa kutolewa. Hata hivyo, huduma za idara hii ni mbovu. Wimbo wa G3 mstari 8 unaonyesha jinsi polisi wanawahangaisha raia mtaani kiasi kwamba hawawezi kulala. Hali ya kawaida ingekuwa raia wanalala usingizi wa pono wakijua kuwa wako salama kwani wanalindwa na polisi. Kinaya ni kuwa hawalali kwa sababu ya kuhofia kupigwa risasi na polisi wakishukiwa kuwa wahalifu.

Isitoshe, wasanii wanadhalilisha idara hii ya polisi kwani polisi wanashirikiana na walanguzi wa zana za uhalifu. Kwa sababu hiyo, vita dhidi ya uhalifu haviwezi kufaulu. Wale ambao wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha uhalifu umekomeshwa ndio

Volume 1, Number 1, 2024 ISSN N0 2791-190Xv

wanawasaidia wahalifu kuuendeleza, kama inavyobainika katika G5 ubeti 7 msitari 17, "*Na polisi wako in cahoots, hao ndio hu supply wagondi na guns za ku shoot*. Polisi wanastahili kujali maslahi ya raia pamoja na kuwatumikia. Hata hivyo, asasi hii inadhalilishwa kwani imewasukuma vijana wengi kushiriki katika matumizi ya mihadarati, pombe haramu na wizi kwani polisi wanakosa kuwajibika katika kupiga vita maovu haya (G5: *Busaa na chwara zinamaliza mayouth)*. Wengi wamejipata kuwa wezi na watumizi sugu wa mihadarati kutokana na utepetevu wa idara hii. Zaidi ya hayo, polisi wanashirikiana na wezi katika wizi kwa kuwapa silaha za wizi ambazo hutumiwa na wahalifu kutekeleza maovu katika jamii. Hivyo basi wanasanii wanadhalilisha idara hii ya polisi kwani badala ya kuangamiza uhalifu wanazidi kuendeleza. Haya yanaafikiana na mawazo ya Njoroge (2014) anayehoji kuwa maafisa wa polisi wana wajibu wa kufanya kazi zao kwa utaalamu na kuonyesha uadilifu katika kila kitu.

Fauka ya hayo, makala haya yamedhihirisha kuwa idara hii inaendelea kudhalilishwa kutokana na vitendo vya polisi kuwahangaisha na kuwaangamiza wanaotetea haki za wanyonge badala ya kutumika kulinda haki zao. Wimbo G5, ubeti 5 (8-9) unadhihirisha hofu ya msanii ya kuuawa usiku kwa kuzindua raia kuhusu hali inayowakumba. Hata hivyo, yeye anasema hataogopa bali yuko tayari kufa kuhakikisha usawa umedumishwa. Kudhalilisha idara hii ya polisi ni dhihirisho polisi hawastahili kuwa na ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa misingi ya rangi, taifa au kabila, lugha, dini, jinsia, umri au kimaumbile bali wanastahili kuwajibika na kuwatumikia raia wote.

### (ii) Jela na Mahakama

Jela na mahakama ni vyombo vya dola ambavyo vimepewa jukumu la kuhakikisha haki imetekelezwa kwa kila mwanajamii. Kwa sababu hiyo, asasi hizi zinapaswa kutekeleza wajibu wao bila mapendeleo wala mwegemeo wowote. Imedhihirika kuwa hali hii haitekelezwi ipasavyo na bila shaka wanasanii wamejitokeza kupinga utendakazi wa vyombo hivi. Vyombo hivi vinajitokeza kama asasi kuu zinazokandamiza maisha ya binadamu hivyo basi vinadhalilishwa. Ingawa vilibuniwa kwa madhumuni ya kusuluhisha matatizo ya binadamu, vinasababisha mateso na mahangaiko mengi sana inavyobainishwa katika matini ifuatayo.

**Matini 2**

***G5 Wajinga Nyinyi* (Ubeti 4, 9-10)**

9. *Ukipelekwa kortini ni escort ya polisi kama sita [*Ukipelekwa kortini unalindwa na polisi kama sita*]*

*10. Iba hizo mamita mmh-scott free, niibe tu kuku ntalala ndani* [iba hayo mamilioni mmh-bila kukamatwa, niibe tu kuku nitalala ndani]

Jela na mahakama ni asasi kuu zinazodhalilishwa katika matini hii. Vyombo hivi vinafaa kutekeleza haki na ni mahali ambapo haki ingefaa kutendwa. Hata hivyo, vyombo hivi vinajitokeza kama asasi kuu zinazokandamiza maisha ya binadamu kama inavyodhihirika katika matini hii. Asasi hizi zinadhalilishwa kwa vile zinafanya kazi kwa hali ya mapendeleo na ubaguzi. Kuna wale wanaoiba mamilioni ya pesa na wanaachiliwa huru. Kinaya ni kwamba wezi wa vitu vidogo vidogo kama vile kuku ndio wanafungwa. Mawazo haya yanafanana na ya Kimugung (2015) anayedai kuwa ingawa vilibuniwa kwa madhumuni ya kusuluhisha matatizo ya binadamu, vinasababisha mateso na mahangaiko mengi huku vikitoa huduma kwa mapendeleo.

### (iii) Bunge

Jukumu la bunge ni uwakilishi wa raia, uangalizi wa utawala na utunzi wa sheria. Ikiwa wabunge hawatatekeleza majukumu haya vilivyo, raia wataathirika pakubwa. Bunge linastahili kuhimiza usawa na haki kwa watu wote kupitia kwa majadiliano na makubaliano ya

Volume 1, Number 1, 2024 ISSN N0 2791-190Xv

wanabunge katika utunzi na utathmini wa sheria ili kusuluhisha matatizo yanayokumba raia wa taifa. Hata hivyo, makala haya yamedhihirisha kuwa asasi hii inapingwa na kudhalilishwa na wasanii wa Muziki wa Kisasa kama inavyoakisiwa katika matini ifuatayo.

**Matini 3**
**G5 *Wajinga Nyinyi***
Ubeti 7 (1-4)
*1. Hapo parliament kwani mnashida gani?* [Hapo bungeni kwani mna shida gani]
*2. Hesabu ya 1 plus 1 inawachenga* [Hesabu ya 1 ongeza 1 inawachenga]
*3. Mtaenda retreat kuidiscuss tena?* [Mtaenda semina kujadili tena?]
*4. Mmetumiwa shetani gani na job ziko wapi?* [Mmetumiwa shetani gani na kazi ziko wapi?

Kinachobainika katika matini hii ni kuwa bunge ni asasi kuu isiyokidhi mahitaji ya raia. G5 ubeti 6 mstari 1 unadhihirisha wazi kuwa wabunge hawajali maslahi ya raia bali hulitumia kuendeleza mahitaji yao. Isitoshe, uwezo wao katika kutekeleza majukumu ya bunge ni wa kutiliwa shaka kwa kuwa hawawezi kuunga moja na moja wakapata mbili. *Hesabu ya 1 plus 1 inawachenga.* Pia wabunge wameshindwa kutimiza ahadi walizoahidia raia kwa manifesto kama vile kubuni nafasi za ajira. Hali hii husababisha ukosefu wa maendeleo na kurudisha taifa nyuma. Mawazo haya yanaoana na maoni ya Njeri (2018) anapohoji kuwa bunge hubadilisha vipengele vya sheria na kutunga vingine ili kuwafaidi walio mamlakani. Kudhalilisha asasi hii ni hatua ya wasanii kuwazindua raia kwa kuwaonyesha kuwa bunge alitimizi wajibu wake na wabunge hawana haja na raia waliowachagua bali haja yao ni kujinufaisha wao wenyewe.

**Matini 4**
**G5 *Wajinga Nyinyi***
Ubeti 5 (5-7)
*5. Nchi inaongozwa na thieves* [nchi inaongozwa na wezi]
*6. Na ukiogopa jua hauwezi kuwa chief* [na ukiogopa huwezi kuwa chifu]
*7. Si mtuibie kiplani* [si mfanye ujanja mtuibie]

Matini hii inadhihirisha kwamba viongozi walio mamlakani ni wezi. Kutokana na hayo raia hawawezi kutarajia maendeleo yoyote kutimizwa kulingana na ahadi za wabunge. Msanii anadhalilisha mchakato wa uchaguzi wa wabunge kwa kuwa raia wenye maadili mema hawawezi kupewa nyadhifa za uongozi kwani wananchi wamezoea viongozi wanaoiba mabilioni ya pesa. Nyadhifa za uongozi zimekuwa daraja la kuelekea kwa uporaji wa mali ya umma. Aidha, viongozi hawa wanafahamu kuwa hamna hatua yoyote inayoweza kuchukuliwa dhidi yao. Viongozi hushamirisha ufisadi maadam raia wanaendelea kunyamaza. Kutokana na hayo, wasanii hawa kwa kudhalilisha asasi hii, wanataka raia wabadilishe hali hii na waanze kuwachagua viongozi wenye maadili mema katika jamii. Isitoshe, inahalisi hatua kali zichukuliwe kwa viongozi fisadi na wang'olewe mamlakani.

Wasanii pia wanadhalilisa bunge linalomilikiwa na wazee kwani wazee wanadumu uongozini milele. Vijana huitwa viongozi wa kesho ilhali wazee wanaendelea kukatalia uongozini. Hata hivyo, wasanii wa Muziki wa Kisasa wanadhalilisha wazo hili kwa kuwahimiza vijana kuwania nyadhifa za uongozi kama inavyojitokeza katika muziki wao. Wasanii hawa wanaonelea kwamba hiyo ndiyo njia ya pekee ya kuhakikisha kwamba kuna mabadiliko katika uongozi kwa kupendekezea wanajamii wachukue hatua zitakazotoa suluhu la matatizo yao. Haya yanalandana na maoni ya Njoroge (2014) kuwa matatizo yanayoikumba jamii yamesababishwa na viongozi waliokatalia uongozini na kuwanyima nafasi vijana kuongoza. Vijana kukaidi hali hii na kujitosa uongozini ni dhihirisho la uanaharakati wa kijamii.

Volume 1, Number 1, 2024 ISSN N0 2791-190Xv

**(iv) Elimu**

Elimu bora humfanya mtu kuhitimu katika taaluma mbalimbali kama vile udaktari, uhasibu, urubani, ualimu, uhandisi, uanasheria na taaluma nyinginezo. Kukosa elimu katika karne hii humtia binadamu katika mikururo ya mikasa (Ogutu, 2021). Mtu yeyote anayezingatia na kuthamini elimu anaweza kusoma yaliyoandikwa vitabuni na wajuzi na wataalamu mbalimbali, kisha akaerevuka na kuishi maisha yatakayomwezesha kukumbana na changamoto za maisha (Kimugung, 2015). Hata hivyo, utafiti huu umebaini kuwa elimu ni asasi kuu inayopingwa na wasanii wa Muziki wa Kisasa. Mtafiti amegundua kuwa licha ya vijana hawa kusoma bado wanakumbwa na changamoto nyingi za maisha na kushindwa kukidhi mahitaji yao muhimu.

**Matini 5**

**G3 *Khalicartel 3* (Ubeti 4, 15-16)**

*15. Industry ngori, yaani ku manoeuvre si ni struggle* [kufanikiwa katika taaluma ni shida sana kwa kuwa sharti mtu apambane]

*16. Interviews, me siko booked, kama libu haina vitabu* [Sijaalikwa mahojiano kana kwamba sikusoma]

**G5 *Wajinga Nyinyi***

Ubeti 3 (1-4)

*1. Fununu ni ati system ya education ni ya uduu* [fununu ati mfumo wa elimu haufai]

*2. Is it true? that's why umepeleka mtoi wako akasome majuu,* [je ni kweli? Ndio maana umepeleka mtoto wako kusomea ng'ambo]

*3. While graduates wanashika placards kwa traffic* [Wakati wale wamehitimu wanabeba mabango barabarani]

*4. Mtu wa actuarial science anataka kujimada, its so tragic* [aliyesomea utakwimu bima anataka kujiua, inasikitisha]

Ubeti 8 (2)

*2. Kazi ni formalities tu, na uki apply ina bounce* [kutuma maombi ya kazi ni utaratibu tu, hata hutafanikiwa]

Matini hii inaonyesha kuwa mfumo wa elimu uliopo hauwasaidii vijana kupambana na changamoto wanazokumbana nazo maishani. Hiki ni kinyume cha matarajio yao kuwa elimu ingewafaidi kwa kuwawezesha kupata kazi. Kwa sababu hii, msanii anasema kwamba mfumo wa elimu uliopo hauna manufaa yoyote kwao. Ingawa vijana walihitimu katika taaluma mbalimbali, taaluma hizo haziwasaidii na wanaendelea kuhangaika kiasi kwamba wengine wanatamauka hadi kuwazia kujitoa uhai. Inashangaza kwa kuwa kijana aliyehitimu hadi chuo kikuu anataka kujiua. Matini hii pia inadhihirisha vile vijana wanaambulia patupu licha ya kutuma maombi ya kazi. Elimu hii isiyo na manufaa kwa vijana inadhalilishwa na wasanii wa Muziki wa Kisasa kwani hata baada ya kusoma hawapati kazi wala kualikwa kwa mahojiano. Kutuma barua za maombi ya kazi ni utaratibu tu usio na maana yoyote. Aidha, makala haya yamebainisha kuwa nyadhifa nyingi za kazi zinatengewa wazee huku vijana wakitengwa na kuwekwa pembeni.

**Matini 6**

**G3 *Khalicartel* 3 ubeti 7 mstari 4**

4. *Bado bado ndani ya ofisi mmejaza ma vitambi.*

**G5 *Wajinga Nyinyi ubeti* 6 (5-8)**

5. *Ni ukweli lazima uretire ndio upate job* [ni ukweli lazima ustaafu ndipo upate kazi]

6. *So inamaanisha lazima kwanza nipatie job, ndio nipate job job?* [kwa hivyo ina maana lazima niwe nimefanya kazi ili niajiriwe?]


Received: 21-07-2024 Accepted: 20-10-2024 Published: 27-12-2024

7. *The youth ni moody at 90 na Gikonyo at 80* [vijana ni Moody akiwa na miaka 90 na Gikonyo akiwa na miaka 80]
8. *Manifesto mlisema job ni plenty* [manifesto mlisema kazi ni nyingi]

Katika matini hii, wasanii wanadhalilisha mfumo wa kusaka ajira kwa kuwa serikali inawabagua na kuwatenga hasa kuhusiana na swala la kazi. Ingawa serikali iliahidi kubuni nafasi za kazi, nafasi hizi hupewa watu wa umri wa makamo au wazee waliostaafu. Dhana inayojitokeza katika G3 mstari 4 ni kuwa wazee wamekatalia ofisini huku vijana wakibaki nyumbani wakisongwa na mawazo tele kwa vile hawana kazi. Wazee wanapoendelea kuongoza, wanawafumba macho vijana kwa kuwapa ahadi za uwongo. Ahadi hizi zinakusudiwa kuwapumbaza wasing'amue kwamba tatizo lao limechochewa na hawa wazee. Moody na Gikonyo ni mifano ya wazee waliwahi kushikilia nyadhifa kubwa serikalini. Hata ingawa walistaafu, waliendelea kupewa vyeo vingine serikalini huku vijana wakinyimwa nafasi yoyote. Haya yanavyojitokeza katika G5 mistari 5-8. Isitoshe, Makala haya yamebaini kuwa mbali na wazee kupewa nyadhifa za kazi, serikali haina mipango kabambe ya kubuni nafasi za ajira. Ipo haja ya serikali kupanua nafasi za kazi ili kukidhi idadi kubwa ya vijana ambao kulingana na matokeo ya Sensa ya mwaka wa 2019, wao ni asilimia sabini ya idadi ya watu wote nchini. Hivyo basi katika hali hii inahalisi serikali kupanua nafasi za kazi ili vijana wapate nafasi hizo.

Vilevile, ukosefu wa ajira unachangia kuchipuka kwa matendo maovu ambapo vijana hulazimika kujiingiza katika uasherati, ulanguzi wa mihadarati pamoja na kucheza kamari ili wapate pesa za kukidhi mahitaji yao ya kimsingi. Hili ni jambo ambalo limefafanuliwa katika matini ifuatayo.

**Matini 7**

**G1 *Kuna Siku Youth Wataungana* ubeti 3 (1-3)**

*1. Ka Sila na Paul, milango ziliji-open* [kama Paulo na Sila milango ilijifungua]
*2. Casino za tao, mipango zao ni all same* [Mipango ya kamari zote za mjini ni sawa]
*3. Nipate, nikose, nisote mpaka nikope*

**G5 *Wajinga Nyinyi* ubeti 3 (12-13)**

*12. Time will tell, Vijana wanabet na Kifo* [Punde si punde uchezaji kamari utawasababishia vijana kifo]
*13. Wanadai betting imewapea job kuwaliko* [Wanadai kucheza kamari kunawapa kazi nzuri kuwaliko]

Imebainika katika matini hii kuwa ukosefu wa ajira umewasukuma vijana wengi katika kushiriki ukahaba na ulanguzi wa dawa za kulevya kama njia ya kujipatia riziki. Katika G1 ubeti 3 mstari1, inadhihirika jinsi vijana wanafurahia kupata nafasi hii ya kucheza kamari. Msanii analinganisha hali hii na furaha waliyopata Sila na Paulo katika Biblia milango ya gereza ilipofunguka. Hawa walikuwa mitume wa Yesu waliofungwa korokoroni kwa kueneza injili. Hata hivyo, usiku wa manane milango ya gereza ilijifungua na wakawa huru. Hivyo basi, vijana kushiriki uchezaji kamari ni mwanya ambao umefunguka wa kutatua matatizo yao (*Ka Sila na Paul, milango ziliji-open).* Imebainika katika makala haya kuwa vijana hushiriki uchezaji kamari bila kujali kama watapata au watapoteza pesa. Mstari 3 unadhihirisha haya anaposema, *Nipate, nikose.* Uchunguzi wa mtafiti umebaini kuwa mchezo huu umewasukuma vijana katika bahari ya madeni kwani inawalazimu wakope ili waendelee kucheza. Hili linajitokeza katika wimbo wa G1 mstari 3 msanii anaposema, *Nisote mpaka nikope.* Matini hii inadhihirisha hali ya kutamausha ambapo vijana wako tayari kufanya lolote hata lile linaloweza kuhatarisha maisha yao katika uchezaji kamari ili wapate pesa. Kushiriki katika matendo haya

maovu ni ishara ya udhalilishaji wa asasi kuu ambazo zimeshindwa kuwanasua vijana kutoka lindi hili la matatizo.

Hali kadhalika, ilibainika katika makala haya kuwa ili kutosheleza mahitaji yao ya kimsingi, vijana wengi wamejiingiza katika ukahaba na ulanguzi wa dawa za kulevya. Mawazo haya yanaoana na ya Ogutu (2015) anayelezea kuwa ukosefu wa ajira umewasukuma vijana wengi katika ukahaba na matumizi ya mihadarati. Mara nyingi mtu ambaye hana la kufanya hutafuta jinsi ya kujiburudisha na kujichumia. Katika hali hii vijana huishia kushiriki katika matendo haya kama kitega uchumi ili kujaribu kubadilisha hali yao ya maisha kama inavyojitokeza katika G1 *(Juu ya madawa, vijana wetu wamepagawa, wasichana wetu kazi wameshindwa, wanagawa).* Hali hii imewasukuma vijana kudhalilisha simulizi kuu na kutafuta njia mbadala za kubadilisha jamii yao.

Kinachobainika katika Makala haya ni kwamba vijana wanalazimika kutumia njia zisizofaa na zisizo halali ili kujikimu kimaisha kama inavyojitokeza katika G1 na G3. Vijana kujiingiza katika uchezaji kamari, ukahaba na ulanguzi wa dawa za kulevya ni udhalilishaji wa asasi kuu. Imedhihirika wazi kuwa vijana hawategemei tena serikali kubuni nafasi za ajira. Wamebuni njia zao za kujipatia pato. Lyotard (1979) alipendekeza matumizi ya simulizi ndogo ndogo zinazosimulia na kuakisi hali halisi ya maisha na kuwa watu watumie urazini na umantiki ili kuleta suluhisho kwa matatizo ya kijamii. Kwa hivyo, uchezaji kamari, ukahaba na ulanguzi wa dawa za kulevya ni nyenzo ambazo vijana wamebuni kusuluhisha matatizo ya kijamii na kiuchumi kama njia ya kudhalilisha serikali kwa vile imeshindwa kupanua nafasi za ajira.

Hivyo basi, elimu inaangaziwa kama isiyosaidia na isiyo na manufaa. Hali hii inaoana na kile Lyotard (1984) alisema kuwa elimu ni mfumo wa maisha wa kipindi cha kisasa ambao ulidhaniwa kuwa ungesuluhisha matatizo ya kijamii. Hata hivyo, mfumo huu unasababisha mahangaiko mengi. Mintarafu ya haya, Lyotard alipendekeza asasi ndogo ndogo zinazoakisi hali halisi ya maisha na hivyo kuleta suluhu. Hivyo basi, wasanii wanawahimiza vijana watie bidii katika taaluma ambazo zinaweza kuwasaidia kupambana na changamoto za maisha kama vile taaluma ya muziki kwani ni nyenzo ambayo ina uwezo wa kuwakwamua kutoka lindi la umaskini (Omari, 2009). Kuwahimiza vijana waendelee kujitahidi katika taaluma hii ya muziki ni udhalilishaji wa asasi kuu kwa vile aina hii ya muziki imefanikisha kuwakwamua kutoka hali mbaya ya uchumi. Isitoshe, kulingana na usasaleo, hii ni mojawapo ya simulizi ndogo ndogo zinazoakisi hali halisi ya maisha ili kuleta suluhisho kwa matatizo ya kijamii. Wakiunga mkono mawazo haya ya Lyotard (1984), Carter (2006) na Barry (2002) wanaelezea kuwa asasi hizi kuu hujidengua na kutafuta njia mbadala. Wengi wa wasanii hawa walikuwa hawana kazi na walikuwa wanashinda mitaani wakijiingiza katika ulevi na uchezaji kamari. Isitoshe, kupitia taaluma hii, vijana wengine wamepata kazi ya utangazaji na uchezaji santuri katika vituo mbali mbali vya redio na televisheni na kumbi za starehe. Hivyo basi, wasanii wa Muziki wa Kisasa, kwa kuwahimiza vijana wajitahidi katika taaluma ya muziki, wanadhalilisha asasi kuu ya elimu na kutafuta njia mbadala ya kusuluhisha matatizo yao. Hivyo basi, serikali inafaa kubuni sera thabiti za kuupiga jeki Muziki wa kisasa badala ya kuupuuza kwani ni chanzo cha ajira kwa vijana wengi.

### (v) Lugha

Wasanii wa Muziki wa Kisasa wanadhalilisha lugha na tamaduni za kigeni kwa kutumia msimbo wa Sheng na lugha za kiasili katika nyimbo zao. Aidha Sheng ni msimbo wa lugha unaowatambulisha vijana kwani unawawezesha kuwasilisha masuala yao. Msimbo huu wa Sheng unaweza kuhesabiwa kama suluhisho la vijana ambao wanachukizwa na jamii iliyogawika katika matabaka, na hali ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili ambazo zina ubaguzi dhidi ya matabaka fulani. Akishadidia mawazo haya, Nabea (2009) anaeleza kuwa lugha ni chombo cha kukuza hejemonia anapoonyesha jinsi lugha ya Kiingereza ilitumika na watu walio

katika tabaka lenye uwezo kutawala wasiojiweza. Udhalilishaji wa asasi hii unajitokeza pale ambapo nyimbo zote zilizochunguzwa zinadhihirisha matumizi ya Sheng hivyo basi kupinga hejemonia ya lugha ya Kiingereza na hata ya Kiswahili. Hii ni ishara ya kutoridhishwa na matumiz yai lugha moja na kuonyesha kuwa lugha zote ni sawa. Aidha wasanii, wanawasuta raia wanaopendelea muziki unaotumia lugha za kigeni na kuchukia muziki wao. Wasanii wanaona kwamba kuchukulia lugha za kiasili pamoja na Sheng kuwa duni ni mtazamo ambao hauna mashiko na unahitaji kutupiliwa mbali. Sharti wenyeji wakuze na kupenda lugha na utamaduni wao. Hili linadhihirika katika matini ifuatayo.

**Matini 8**
**G2 Kwendaa *(*kibwagizo 1-5)**
*1. Sipendi mangoma za Kenya (Kwenda! Kwenda!)*
*2. Mi sitambui Omollo (Kwenda! We kwenda!)*
*3. Ah, si huyu boy huringa? (Kwenda! Kwenda!)*
*4. Mi sijawahi hire madinga (Kwenda! Shenzi!)*
*5. Ah, mi sipendi hizo mangoma (Kwenda! Kwenda!)*

Kinachobainika katika matini hii ni kuwa wasanii wanapinga kasumba za kigeni kama asasi kuu. Wanawasuta wale ambao wanachukia muziki wa wasanii wa hapa nchini Kenya na kupigia upatu muziki wa kigeni. Kulingana na Njogu na Chimera (1999), lugha ya Kiingereza na fasihi, zikiwemo nyimbo, ni vyombo vya ukandamizaji. Ili kuwapumbaza Waafrika, wakoloni walionyesha Waafrika kuwa utamaduni wao ulikuwa ni ushenzi na kwa hivyo kuwarai wakumbatie mafunzo ya kigeni. Lugha za Kiafrika zilichukuliwa kuwa duni (Ngugi, 1986). Mwafrika alishawishiwa kuwa utamaduni wake ni wa kishenzi. Waafrika walirithi baadhi ya tamaduni za kigeni na kuchukia tamaduni zao. Hivyo basi, wasanii wa Muziki wa Kisasa kupinga hali hii ni ishara ya udhalilishaji wa asasi kuu. Aidha, Makoni na wenzake (2010) wanahoji kuwa Waafrika kuendelea kupendelea lugha na tamaduni za kigeni ni kujirudisha katika minyororo ya kikoloni. Anaelezea kuwa hii ni asasi kuu ambayo haitaleta suluhisho la matatizo yanayowakumba Waafrika. Anadai kuwa suluhisho la uelewa mwafaka wa fasihi ya Waafrika litapatikana iwapo Waafrika watatumia lugha zao kuendeleza fasihi yao zikiwemo nyimbo.

Isitoshe, wasanii wanapochanganya lugha mbili au zaidi katika tungo, wanataka lugha zao zipewe nafasi katika jamii ikiwemo Sheng. Isitoshe, hii ni ishara ya kutaka kujikomboa kutokana athari za ukoloni mamboleo ambapo lugha moja ilionekana kuwa bora kuliko lugha zingine. Kwa mantiki hii, wasanii wa Muziki wa Kisasa wanajitokeza kuwa wanaharakati ambao wanatetea usawa wa lugha katika jamii ikiwemo lugha ya Kiswahili ambayo imetambulika duniani kote. Wanataka kuona jamii ambamo hakuna lugha inayochukuliwa kuwa bora kuliko nyingine. Haya yote yanabainisha kuwa wanadhalilisha matumizi ya lugha moja katika sanaa.

**(vi) Dini**
Dini ni kipengele cha asasi kuu kinachodhalilishwa na wasanii wa Muziki wa Kisasai. Utafiti huu umebaini kuwa badala ya viongozi wa dini kuwapa raia matumaini ya kuendelea kuishi na kuhimiza watu kuwa waadilifu katika jamii, wanahusika katika kuendeleza maovu katika jamii. Haya yanaoana na maoni ya Ogutu (2015) anapolezea kuwa dini inafaa kuwa msaada kwa wanajamii badala ya kuwa kitovu cha mahangaiko yao.

Udhalilishaji wa asasi ya dini unabainika pale ambapo wasanii wanapinga uzandiki wa viongozi wa kidini. Wasanii wanawakashifu viongozi hawa kwa ajili ya tamaa yao ya pesa inayowakandamiza raia kwani kila mara wanahitajka kutoa sadaka au fungu la kumi (G4: *Waumini…kushoto fungu la kumi, sadaka kulia)*. Ni wazi kuwa dini ni kikwazo kikubwa cha


**Received: 21-07-2024 Accepted: 20-10-2024 Published: 27-12-2024**

Volume 1, Number 1, 2024 ISSN N0 2791-190Xv

maendeleo ya jamii kwani ni nyenzo ya kuwanyanyasa raia na ni kimbilio la viongozi fisadi wanaopokelewa kwa mikono miwili na viongozi wa dini (G4: *Ndio maana mbele ya kanisa mheshimiwa anakula sakramenti kabla ya raia).* Inasikitisha kuona viongozi wa dini wakifurahia kupokea pesa za ufisadi huku waumini wao wakishangilia. Viongozi hawa wanatumia mahudhurio ya makanisa kama jukwaa la kuonyesha kwamba hakuna maovu yanayoendelezwa na utawala wao. Haya yanadhalilishwa na wasanii kwani suluhisho la maovu ya jamii yanastahili kupatikana kupitia kwa dini wala si dini kuendeleza maovu haya. Ogutu (2021) anakubaliana na mawazo haya anapoelezea kuwa dini ni chombo kinachotumiwa kuwadhulumu waumini na raia kwa jumla. Ikiwa hili halitakomeshwa bila shaka vijana watakosa wale ambao watakuwa vielelezo vya maadili kwao ili kuwawezesha kutimiza ndoto zao.

**Hitimisho**

Makala haya yamethibitisha kuwa nyimbo zilizochanganuliwa zimetumika kudhalilisha asasi kuu za kijamii kwa vile zinasababishia raia mahangaiko mengi. Asasi kuu zinazopingwa katika Muziki huu wa Kisasa ni pamoja na vyombo vya dola, elimu, dini na lugha. Hii ni kwa sababu asasi kuu hazina uhusiano wowote na hali halisi ya maisha. Udhalilishaji huu umeibua mitazamo na hatua tofauti za kusuluhisha changamoto zinazokumba jamii ya usasaleo na hivyo basi kuboresha maisha ya vijana. Kwa hivyo, wasanii wanaendekeza matumizi ya asasi ndogo ndogo zinazosimulia na kuakisi hali halisi ya maisha ya vijana kama vile kujitosa katika uimbaji wa muziki wao wa kisasa.

**Maraejeleo**


Barry, Peter. (2002). *Beginning theory*. Manchester University Press.

Carter, D. (2006). *Literary theory*. Cox & Wyman.

Gromov, M. (2022). Depiction of the younger generation in Kenyan Swahili women's prose in the twenty-first century. *The Nairobi Journal of Literature*. http://uonjournals.uonbi.ac.ke/ojs/index.php/literature/index SSN 1814-1706-1081. Number 10 (Special Issue), May, 2022

Kasyoka, E. (2022). *An analysis of 'problematic contents' expressed in gengetone songs in Kenya*. Unpublished. M.A. Research Project submitted to the University of Nairobi.

Khakasa, M. S. (2016). *Matumizi ya rasilimali za kiswahili za mtandao wa kiakademia na wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Maseno.

Kimugung, S. (2015). *Mitindo mamboleo ya ubaadausasa katika nyimbo teule za jamii ya Kikalenjin za karne ya ishirini na moja*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Moi.

Kiongera, K. (2010). *Mchango wa vijana katika mabadiliko chanya katika tamthilia nne za Kiswahil*i. Tasnifú ya Uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Kipkemoi, R. A. (2018). *Simulizi za virusi vya ukimwi/ukimwi zinavyodhihirika katika nyimbo za jamii za Kenya kibaadausasa*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa Iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Moi Eldoret.

Kipsang, F. (2021). *Most popular sheng words 2020 and their meanings*. The Saturday Standard.

Koech, L. (2021*).* Relationship between watching 'Gengetone' music and drug abuse among the youth in Uasin Gishu County, Kenya. *East African Journal of Interdisciplinary Studies, 3*(1) 103-115.

Lyotard, J. (1979). *The postmodern condition: a report on knowledge.* Manchester University Press

Lyotard, J. (1984). *The postmodern condition. A report on knowledge.* Trans. Geoff Bennington and Brian Massuni. Minneapolis: University of Minnesota Press.

Makoni, S., Makoni, B., Rosenberg, A. (2010). The wordy worlds of popular music in Eastern and Southern Africa: Possible implications for language-in-education policy. *Journal of Language, Identity, and Education, 9(*1) 1–16

Mukasa, A. (2022). Gengetone music as a subversion of the urban space. *Journal of Creative Arts, Communication and Media Studies Volume 1,* Issue 1, 2022 ISSN: 2958-1737 (Print) ISSN: 2958-1745 (Online)

Newmark, P. (1991). *About translation.* Multilingual Matters Ltd.

Nabea, W. 2009. 'Language policy in Kenya: Negotiation with hegemony'. In: Itibari, Zulu (Ed.) *Journal of Pan African Studies*. Los Angeles, (3) 1, 121-138.

Ngugi, M. (2000). Nafasi ya muziki uliopendwa katika fasihi ya Kiswahili. *Swahili Forum, VII,* 145-152.

Ngugi, T. (1986). *Decolonising the mind. The politics of language in African Literature*. James Currey.

Njeri, W. (2018). *Mchango wa vijana wa kuleta ukombozi katika yasinya, zinguo la mzuka na mwavyaji*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, A.W. (2014). *Viongozi kama Visababishi ya Mabadiliko katika Riwaya za Mwenda Mbatia. T*asnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ogutu, H.O. (2015). *Changamoto za Vijana katika Riwaya Teule za Ken Walibora.*Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Laikipia.

Ogutu, H.O. (2021). *Uhimili wa hejemonia na nafasi ya vijana katika riwaya teule za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa iliyowasilishwa katika Chuo Kikuu cha Laikipia

Omari, S. (2009). Muziki wa hip hop na bongo fleva katika kuhamasisha usomaji. *Mulika, Toleo maalum*, 100-111

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Focus.

Wanjala, H. (2016) *Popular music and identity formation among Kenyan youth* Muziki 13(2):20-35 DOI:10.1080/18125980.2016.1249159

Walmsley, C. (2006). Postmodernism. In Patricia Waugh (Ed.) *Literary theory and criticism*: *An Oxford guide* (405 – 426). Oxford University Press.


Received: 21-07-2024 Accepted: 20-10-2024 Published: 27-12-2024